/ISSN 0856 – 0331X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

*No. 1.* *28 Januari, 2025*

*SPECIAL SUPPLEMENT*

*To The Special Gazette of the United Republic of Tanzania No. 1. Vol. 106 Dated 28 Januari, 2025*
Printed by The Government Printer, Dodoma by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI Na. 50A la tarehe 28/1/2025

SHERIA YA KODI YA MAPATO,
(SURA YA 332)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 10)*

AMRI YA MSAMAHA WA KODI YA ZUIO KWENYE RIBA YA MIKOPO KUTOKA TAASISI ZA FEDHA ZA KIGENI KATIKA MRADI WA UANZISHWAJI WA KILIMO CHA MIWA NA UENDESHAJI WA MTAMBO WA KUZALISHA SUKARI WA KAMPUNI YA MTIBWA SUGAR ESTATE YA MWAKA 2025

Jina na kuanza kutumika

**1**. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Kodi ya zuio kwenye Riba ya Mikopo Kutoka Taasisi za Fedha za Kigeni katika Mradi wa Uanzishwaji wa Kilimo cha Miwa na Uendeshaji wa Mtambo wa Kuzalisha Sukari wa Kampuni ya Mtibwa Sugar Estate ya Mwaka 2025 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika tarehe 28 Juni, 2024.

Msamaha

**2**. Kodi ya zuio kwenye riba itokanayo na mikopo kutoka taasisi za fedha za kigeni kwa Kampuni ya Mtibwa Sugar Estate katika utekelezaji wa mradi wa Uanzishwaji wa Kilimo cha Miwa na Uendeshaji wa Mtambo wa Kuzalisha Sukari inasamehewa.

Ukomo

**3**. Amri hii itafika ukomo wake tarehe 27 Juni, 2028 na inaweza kuongezewa muda kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa utekelezaji baina ya Kampuni ya Mtibwa Sugar Estate na Kituo cha Uwekezaji Tanzania kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa tarehe 25 Machi, 2022.

Dodoma,
31 Disemba, 2024

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha*